

7. Kotesheni zote katika uhalisia wake (Original) pamoja na nakala moja zinazofanana na zilizojazwa kwa usahihi, kusainiwa kwa mkono na kuwekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi na kuandikwa **LGA/145/2021/2022/W/09** juu ya bahasha pamoja na anwani **KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA WILAYA NYASA, S.L.P 90, MBAMBA BAY.**
8. Siku ya mwisho ya kuwasilisha kotesheni ni tarehe **29/04/2022** siku ya Ijumaa kabla ya saa 06:30 mchana. Kotesheni zote zitarejeshwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya wilaya Nyasa- Kitengo cha Manunuzi ( Kilosa Bomani) kabla ya muda wa mwisho ulioainishwa.
9. Ufunguzi utafanyika mara moja baada ya muda wa mwisho ulioainishwa hapo juu, mbele ya Mafundi au wawakilishi wao walioamua kuhudhuria katika ufunguzi wa kotesheni za mradi wa kutengeneza nguzo za barabara kwa ajili ya anuani za makazi.
10. Maombi yatakayochelewa, Maombi yasiyo kamilika, Maombi ambayo hayatakuwepo siku ya ufunguzi, hayatapokelewa na kuhusishwa katika zoezi la uchambuzi wa kumpata fundi atakae fanya kazi ya Ujenzi.

N.B: Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya halmashauri ya wilaya Nyasa ([www.nyasadc.go.tz](http://www.nyasadc.go.tz))

  
Emmanuel Kapinga  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
